LIC LOCAL INVESTMENT CLIMATE

Brief No. 12

VIJANA NA KILIMO BIASHARA (KIGOMA NA DODOMA)

Mradi wa kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji (LIC) ni mradi wa kuendeleza sekta binafsi unaofadhiliwa na Danida. Mradi unashughulikia vikwazo vikuu vinavyokwamisha maendeleo ya biashara na ukuaji wa uchumi katika ngazi ya wilaya kwenye mikoa miwili ya Dodoma na Kigoma nchini Tanzania. LIC imejikita katika mijadala kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, miundombinu ya utoaji wa huduma za biashara ikiwa ni pamoja na vituo vya pamoja vya biashara na miundombinu ya pamoja kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kusaidia maendeleo ya biashara na uwekezaji. Washirika wanaotekeleza mradi wa LIC ni Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Sekretariati za mikoa ya Kigoma na Dodoma, Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) Tanzania, Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT), Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Chemba ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Vijana na Biashara - Changamoto na dhana

Vijana wanaotaka kuingia katika biashara - ikiwa ni uzalishaji katika kilimo au usindikaji /viwanda – wanakabiliwa na changamoto kadhaa mwanzoni. Elimu rasmi na mafunzo ya ufundi wanayopata yanakuwa na ukosefu wa mbinu za kibiashara na vyeti au stashahada wanazozipata hazikopesheki. Hivyo basi, kupata nyenzo za uzalishaji ikiwa ni pamoja na mtaji ni changamoto kubwa. Zaidi ya hayo, katika wilaya nyingi, hakuna miundo au taasisi saidizi ambapo vijana wanaweza kupata msaada juu ya usimamizi wa biashara.

Dhana hii ya vijana katika biashara chini ya programu ya LIC ina lengo la kusaidia vikundi vya vijana vilivyoanzishwa kwa nia ya kufanya biashara. Msaada unajumuisha kusaidia kuandaa mipango biashara, kujenga uwezo katika usimamizi wa biashara na mtaji wa kuanzia. Kundi lengwa ni vijana mwenye elimu ya ufundi lakini hawana matarajio ya kweli ya kutafuta elimu ya juu. Makundi ya vijana yana mawazo na ari na kwa kushirikiana na LIC watajenga msingi mzuri. Makundi hayo yatakuwa mfano na yatahamasisha vijana wengine kuchukua/kukabiliana na changamoto na fursa.

Uwekezaji wa LIC kwa vijana katika biashara

Kwasasa, LIC inasaidia makundi kadhaa ya vijana katika mikoa ya Dodoma na Kigoma. Mkoani Dodoma, LIC imesaidia kituo cha kilimo cha kata ya Kibakwe na inaendeleza kituo cha mafunzo ya usindikaji kwa kulenga vijana wenye elimu ya msingi tu. Mkoani Kigoma, kundi la vijana linalojishughulisha na kilimo cha maua na mbogamboga na ufugaji wa kuku limeanzisha mabwawa ya samaki na linaanzisha pia mgahawa hapo mkoani Kigoma. Kundi jingine litazalisha vifaranga vya samaki kwa ajili ya uzalishaji wa bwawa la samaki. Hata hivyo makundi mengine yanajitokeza katika kilimo cha maua na mbogamboga, ufugaji wa kuku na kuendesha migahawa huko Kasulu, Kibondo na Uvinza.

Vijana wakiandaa kitalu cha miche ya mitende

Mtaalamu wa kilimo, Kigoma

Mapendekezo ya jinsi ya kuendelea mbele na programu hii ya vijana na biashara



Kijana akifanya kazi katika shamba la Big Power, Kibondo-Kigoma

Vijana wakiwa wamesimama na mshauri kutoka Big Power, Kibondo-Kigoma

Ili kukabiliana na ukosefu /upungufu wa mashirika yanayotoa uangalizi/ufuatiliaji na msaada kwa vijana wanaotaka kuanza biashara pamoja na kukabiliana na mapungufu ya taasisi za kifedha katika kusaidia vijana, mambo muhimu ambayo mradi wa LIC umejifunza kupitia mazungumzo mapana na mbalimbali wadau wa mradi, imepelekea mapendekezo yafuatayo:

1. Katika ngazi ya Mkoa, chombo maalum cha uendeshaji (SPV) kinapaswa kuundwa kwa kushirikiana na vyombo husika vya serikali, taasisi husika za elimu za mikoa, jumuiya ya wafanya biashara na wawakilishi wa vijana ili kuweza kusaidia vijana wenye lengo la kuingia katika biashara. Lengo la SPV hii ni kukusanya fedha, kutoa msaada wa kiufundi ikijumuisha kujengea uwezo wa kuendesha biashara, ukaguzi wa mahesabu na ushauri wa kisheria.

2. Kila halmashauri /manispaa katika wilaya kuanzisha SPV ya vijana na biashara ikiwa na uwakilishi wa wadau wa eneo husika kutoka sekta ya umma na sekta binafsi. Lengo ni kushughulikia changamoto katika ngazi ya wilaya kwa vijana wanaoingia kwenye biashara na kwa kushirikiana na SPV ya Mkoa kutoa huduma zinazohitajika

3. Kila wilaya kutenga eneo la ardhi (ekari 3-5) kwa ajili ya kituo cha biashara cha vijana. Kituo hiki kinapaswa kuwa na bweni dogo na darasa (kama hakuna taasisi nyingine inayoweza kutoa hizo huduma), vifaa vya usindikaji kwa ajili ya majaribio ya usindikaji mdogo, vitengo vya mafunzo ya kilimo cha maua na mbogamboga, ufugaji wa kuku, bwawa la samaki, au chochote kinachofaa kwa wilaya husika na kitu kingine chochote cha muhimu na maslahi kwa vijana - kama vile mgahawa, ambacho kinafurahisha na pia ni mazingira mazuri ya kujifunza jinsi ya kuendesha biashara.

4.Kikundi cha vijana kilichosajiliwa katika ngazi ya wilaya na wanaotaka kujiunga na programu ya vijana na biashara wataunganishwa na kituo cha biashara cha vijana na kufuata taratibu zilizowekwa ili waweze kupata msaada na ushiriki.

5. Baraza la biashara la vijana litaanzishwa katika ngazi ya wilaya likiwa na uwakilishi kutoka kwenye makundi yote ya vijana wanaohusika. Baraza hili litawakilisha wafanyabiashara vijana kwa upande mmoja na mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingine husika kwa upande mwingine na watachagua /kuteua wanachama wataoingia kwenye chombo cha SPV katika ngazi ya wilaya na mkoa.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti ya mradi wa LIC: www.lic.or.tz

Februari 2019